



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU
WAKALA WA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI (OSHA)



TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI LINARUDIWA

Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi ni Taasisi ya Serikali iliyoungwa kwa mujibu Sheria ya Wakala wa Serikali Namba **30** ya mwaka **1997** ambapo majukumu yake yameainishwa katika Sheria Ya Usalama na Afya Mahali Pa Kazi Namba **5** ya Mwaka **2003**. Wakala pamoja na kazi nyingine una dhamana ya kusimamia Usalama na Afya za Wafanyakazi wanapokuwa kazini.

Ili kuhakikisha kuwa Wakala unatekeleza Majukumu kama yalivyoainishwa katika sheria tajwa hapo juu, Mtendaji Mkuu anakaribisha maombi kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi zipatazo Kumi na nane **(18)** za **Mkataba wa miaka mitatu (3) kwa** Kada tofauti kama ifuatavyo;

1.0 DEREVA II (NAFASI 10)

1.1 SIFA ZA WAOMBAJI

- i.** Awe na cheti cha kidato cha nne **(Form IV)**
- ii.** Awe na leseni ya Daraja la **E** au **C1** ya uendeshaji magari.
- iii.** Awe na uzoefu usiopungua mwaka mmoja **(1)** bila kusababisha ajali.
- iv.** Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari **(Basic Driving Course)** yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi **(VETA)** au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- v.** Waombaji wenye cheti cha Majaribio ya Ufundi Daraja la II wataanza kufikiriwa.

1.2 MAJUKUMU YA KAZI

- i.** Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- ii.** Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kazi.
- iii.** Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari.
- iv.** Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
- v.** Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
- vi.** Kufanya usafi wa gari.
- vii.** Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

1.3 MSHAHARA

OSHA 3.1 kwa mwezi.

2.0 MTUNZA KUMBUKUMBU MSAIDIZI (*NAFASI 4*)

2.1 SIFA ZA WAOMBAJI

- i. Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne (*IV*) au cha Sita (*VI*).
- ii. Awe amehitimu mafunzo ya Utunzaji wa Kumbukumbu katika ngazi ya Cheti katika mojawapo ya fani ya Masjala kutoka katika vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.

2.2 MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kutafuta Kumbukumbu, nyaraka na Majalada yanayohitajiwa
- ii. Kuthibiti upokeaji na uandikishaji wa Kumbukumbu
- iii. Kuchambua, kuorodhesha na kupanga Kumbukumbu
- iv. Kufungua Majalada mapya yanayohitajika.
- v. Kuweka Kumbukumbu (*barua, nyaraka, n.k*) katika Majalada
- vi. Kuweka/kupanga kumbukumbu/nyaraka katika makabati na reki (*file racks/cabinet*) katika masijala.
- vii. Kuthibitisha Machapisho kwa ajili ya Kumbukumbu za ofisi ndani ya muda uliopangwa
- viii. Kutoa elimu ya mara kwa mara kwa Maafisa wanaokiuka utaratibu wa uhifadhi wa Kumbukumbu.
- ix. Kufanya kazi nyingine atakayopangiwa na Msimamizi wake.

2.3 MSHAHARA

OSHA 3.1 kwa mwezi.

3.0 MHASIBU MSAIDIZI (NAFASI 4)

3.1 SIFA ZA WAOMBAJI

- i.** Awe na Stashahada ya Kawaida ya Uhasibu (*Diploma in Accountancy*) kutoka Chuo/Taasisi yoyote inayotambuliwa na Serikali.
- ii.** Awe na cheti cha ufaulu mtihani mgumu wa Uhasibu Serikalini (*Higher Standard Government Accountancy Examination*) unaotolewa na Chuo cha Utumishi wa Umma.
- iii.** Awe na uzoefu usiopungua mwaka mmoja (**1**) katika fani ya Uhasibu.

3.2 MAJUKUMU YA KAZI

- i.** Kupokea na kulipa fedha.
- ii.** Kutunza Daftari la fedha.
- iii.** Kufanya usuluhisho wa hesabu za benki. (*Bank Reconciliation*)
- iv.** Kukagua hati za malipo.
- v.** Kupitisha malipo kulingana na Kanuni za fedha.
- vi.** Kusimamia kazi za Wasaidizi wa Hesabu.
- vii.** Kufanya kazi nyingine atakayopangiwa na Msimamizi wake.

3.3 MSHAHARA

OSHA 4.1 kwa mwezi.

4.0 MASHARTI YA JUMLA

- i.** Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka Arobaini na Tano (**35**)
- ii.** Waombaji waambatishe Cheti cha kuzaliwa.
- iii.** Maombi yaambatane na picha moja ya mwombaji ya hivi karibuni (passport size)
- iv.** Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**CV**) yenye anwani na namba za simu pamoja na majina ya wadhamini watatu (**3**).
- v.** Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.

- vi. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (*TCU/NECTA*).
- vii. Watakaowasilisha taarifa na sifa za kugushi watachukuliwa hatua za kisheria.
- viii. Maombi yatumwe kwa njia ya Posta au kwa mkono kufikishwa Ofisi za Makao Makuu zilizopo Kinondoni Barabara ya Mahakama.
- ix. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe *29/12/2017*.
- x. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa hayatafanyiwa kazi.

1.5 JINSI YA KUWASILISHA MAOMBI

Maombi yote yatumwe kwa;

**Mtendaji Mkuu,
Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi,
S.L.P 519,
DAR ES SALAAM.**

